

# COVID-19

## ALIGHT INAFANYA NINI?

Alight iko kwenye mstari wa mbele –  
kukomesha maambukizi ya virusi vya korona katika nchi zote 19 tunazofanya kazi. Lengo  
letu ni kuwalinda watu – jamii zetu, wafanyakazi wetu, na watu tunaowahudumia. Hii ni  
miongozo michache kutoka kwa Shirika la Afya Duniani (WHO).

### NI KWA NJIA GANI BORA ZAIDI TUNAWEZA KUJIKINGA?

Kuzuia maambukizi ndiyo njia bora zaidi – virusi hivi vinaweza kuambukizwa hata bila kuonyesha dalili zozote. Ili kusaidia kukomesha maambukizi:

- Nawa mikono yako kila mara (kwa sekunde 40-60 kwa kiwango cha chini)
- Tumia sanitaiza (yenye 70% ya pombe au zaidi)
- Dumisha umbali wa mita moja kutoka kwa jirani yako ukiwa katika umati wa watu.
- Epuka kushikashika uso wako.
- Tumia karatasi shashi au kiwiko cha mkono wako unapokohoa au kupiga chafya.

### DALILI ZA UGONJWA HUU NI ZIPI?

Dalili za kijumla za ugonjwa huu ni pamoja na:

- Joto jingi mwilini
  - Uchovu
  - Kikohozi kikavu
- Na wakati mwingine
- Maumivu ya viungo vya mwili
  - Kutokwa na makamasi
  - Koo lililokauka
  - kuendesha

Watu wengine hawaonyeshi dalili yoyote wala kuhisi wagonjwa.

### NI KWA NJIA GANI BORA ZAIDI TUNAWEZA KUZILINDA JAMII ZETU?

Tunastahili kuhakikisha **kutotangamana kwa karibu**, ambako kunajumuisha kupunguza idadi ya watu tunaoCAA pamoja nao – tunapogusana na watu wachache, ndivyo ilivyo idadi chache ya watu wanaoambukizwa.

- Jiepushe na mikutano isiyo muhimu
- Nawa mikono yako na uepuke kushikashika uso wako au watu wengine
- Ukiwa katika umati wa watu, jaribu kudumisha umbali wa mita moja kutoka kwa jirani yako
- Kuwa mwangalifu unapotangamana na watu walio kwenye hatari ya kuambukizwa kiraishi
- Zaidi ya yote, dumisha usafi, na iwapo unahisi mgonjwa, mpigie simu mhudumu wa afya!

### NANI ANASTAHILI KUWA MWANGALIFU ZAIDI?

Kijumla, dalili za ugonjwa huu ni za kiwango cha chini. Kisa 1 hadi 5 ndivyo huwa vya kuitiliwa maanani (huhitaji mgonjwa kupelekwa hospitalini).

COVID-19 huwaathiri zaidi:

- Wazee
- Watu walio na matatizo mengine ya kiafya kama vile magonjwa ya moyo, kisukari, magonjwa ya mapafu na mfumo wa kupumua, na HIV
- Wanawake wajawazito wanastahili pia kuwa waangalifu.

### UNASTAHILI KUFANYA NINI IWAPO MTU NI MGONJWA?

- Wasiliana na mhudumu wa afya kwa ushauri na usaidizi, kwa kumpigia simu
- Kadri inavyowezekana, usimruhusu mgonjwa kwenda kumwona mhudumu wa afya kwenye kliniki au kwenda kwenye maeneo ya umma
- Iwapo unamsaidia mtu aliye na dalili za ugonjwa huu, hakikisha unanawa mikono, na iwapo unazo, vaa barakoa na glavu

### JE KUNAYO CHANJO?

Hakuna chanjo bado; hata hivyo, watafiti wanajitahidi kuitengeneza chanjo hiyo na inaweza kuchukua zaidi ya mwaka mmoja ili kuwa tayari. Hata hivyo, kuzuia ndilo chaguo bora zaidi.